

**NOVENA YA TATU (3) KWA MAANDALIZI YA SAFARI YA HIJA
KIBEHO RWANDA.**

NOVENA KWA BIKIRA MARIA WA MSAADA WA DAIMA

TAREHE 24-FEB....03-MACHI-2020



1.SALA YA MWANZO:

Ee Maria, Mama wa Msaada wa kudumu, ambaye unatuangalia kwa upendo kutoka katika picha hii ya muujiza, tunakukimbilia wewe kwa matumaini ya kitoto tukikuletea maombi yetu. Utuanagalie sisi kwa wema na uyasikilize maombi yetu. Utusaidie katika mahitaji yetu mbalimbali. Tunakuomba hayo kwa nguvu na moyo wote.Amina

2. SALA YA UJE ROHO MTAKATIFU AU UTENZI WA UJE ROHO MTAKATIFU.

3. Ee Bikira Maria wa Msaada wa Kudumu,

Ninakuja leo mbele ya picha yako takatifu kwa matumaini makubwa mno, ili kuomba msaada wako. Sizitegemei stahili zangu wala matendo yangu mema, bali ninazitegemea stahili zisizo na mwisho za Bwana Yesu na upendo wako mkuu wa kimama. Wewe ee Mama, uliyaangalia madonda ya Mkombozi na Damu yake iliyomwagika msalabani kwa ajili ya wokovu wetu. Huyo Mwana wako wakati wa kufa alituachia wewe uwe Mama yetu. Uwe basi kwetu, kama inavyosema jina lako tamu: Msaada wa kudumu. Basi, kwa ajili ya maumivu makali na kifo cha Mwana wako, kwa ajili ya mateso yasiyoelezeka ya moyo wako, ninakuomba sana wewe, ee Mama wa msaada wa kudumu, unionbee mbele ya Mwana wako neema ninayoitamani na ninayohitaji sana.....(hapa taja ombi lako). Wewe unajua, ee Mama Mbarikiwa sana, jinsi gani Yesu Mwokozi wetu anataka kutujalia matunda yote ya wokovu. Wewe unajua, kwamba hazina hizi zimewekwa mikononi mwako, ili utugawie sisi. Unionbee ee Mama Mwema sana kwa Moyo Mtakatifu wa Yesu neema hii ninayoomba kwa unyeneyekevu katika novena hii, na mimi nitaisifu kwa furaha huruma yako milele.

4. Maombi

Kiongozi: Ee Maria, uyasikilize maombi yetu!

Kiitikio: Tunakuomba, ee Bikira Maria wa Msaada wa Kudumu!

Kwa wagonjwa, ili uwaponye. ***Kiit.***

Kwa wenyewe huzuni, ili uwafariji. ***Kiit.***

Kwa wanaaoomboleza, ili uyaafute machozi yao. ***Kiit.***

Kwa yatima na walioachwa , ili uwe mama kwao. ***Kiit.***

Kwa maskini na wenyewe mahitahi, ili uwasaide . ***Kiit.***

Kwa wanaopotea, ili uwarudishie kwenye njia ya ukweli. ***Kiit.***

Kwa wanaoshawishiwa, ili uwaokoe na mitego ya shetani. ***Kiit.***

Kwa wanaoanguka, ili uwahimize kwenye kutenda mema. ***Kiit.***

Kwa wakosefu, ili uwajalie neema ya toba na kitubio. ***Kiit.***

Uyasikilize maombi yetu yote. ***Kiit.***

Shukrani

Kiongozi: Ee Maria, uzipokee shukrani zetu!

Kiitikio:Tunakushukuru, ee Bikira Maria wa Msaada wa Kudumu!

Kwa wagonjwa waliopona. ***Kiit***

Kwa wenyewe huzuni waliofarijija. ***Kiit.***

Kwa waliookolewa na kukata tamaa. ***Kiit***

Kwa waliookolewa na nguvu ya dhambi. ***Kiit***

Kwa waliosikilizwa katika kuomba. ***Kiit.***

Kwa huruma uliyotuonyesha. ***Kiit***

Kwa upendo wako wa kimama. ***Kiit.***

Kwa wema wako mkuu sana. ***Kiit.***

Kwa neema zote ulizotujalia sisi na kwa wengine. ***Kiit.***

5. PIA TUSALI ROZARI YA MATESO SABA YA BIKIRA MARIA.

6. SALA YA KUFUNGIA TUNAKIMBILIA ULINZI WAKO.

NB; Sala ya Novena ni hii hii Siku zote 9 **Haibadiliki.**